

"HUDUMA ZA RITA NI MUHIMU KWA MAENDELEO YA TAIFA"- Mhe. Dr. Mwakyembe.



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dr. Harrison Mwakyembe amesema kwamba Huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa lolote Duniani ikiwemo Tanzania. Aliyasema hayo Jana alipotembelea Ofisi za RITA Makao Makuu jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujionea Wakala unavyotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Waziri aliwaeleza Wafanyakazi wa RITA kwamba Wakala unalo jukumu Muhimu sana kwa Taifa la kuchukua na kutunza taarifa za matukio za muhimu ya matukio ya Wananchi na taarifa hizo kuweza kutumika kupanga mipango ya Maendeleo. "Duniani kote maendeleo ya nchi yanaonekana kuititia uwepo wa taarifa za matukio muhimu ya wananchi wake ambazo huhiwezesha Serikali kupanga mipango madhubuti ya Maendeleo na kutoa huduma" alisema Waziri Mwakyembe.

Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Waziri alipata nafasi ya kutembelea Vitengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Usajili, TEHAMA na Utunzaji wa nyaraka kujionea Wakala unavyotekeleza majukumu yake kwa Vitendo. "Naipongeza sana RITA kwa kuweza kuboresha huduma zake kwa kuanza kutumia teknolojia ambayo imeongeza ufanisi kuwezesha wananchi kupata vyeti nya kuzaliwa ndani ya Siku 7 tofauti na zamani ilipokuwa ikichukua zaidi ya miezi mitatu" alisema Waziri Mwakyembe.

Vile vile Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Bi Angela Anatory alipata fursa ya kusoma Taarifa ya Wakala iliyojumuisha utekelezaji Majukumu, mapato na matumizi, mikakati na changamoto zinazoukabili Wakala.

Katika taarifa hiyo, Bi. Angela alitoa ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu Mkakati wa Kuboresha Mfumo wa Kukusanya na kutunzaji Takwimu za Matukio Muhimu kwa Mwanadamu (*Civil Registration and Vital Statistics*) ulio katika hatua za awali za maandalizi ya utekelezaji ambao lengo lake kubwa ni kusogea huduma za Usajili wa matukio haya karibu na makazi ya wananchi. Matukio makuu muhimu kwa mwanadamu ni Kizazi, Kifo, Ndoa na Talaka.

Akiongea na Wafanyakazi, Mheshimiwa Waziri alisema ataendelea kushirikiana kwa karibu na RITA katika kuzitafutia ufumbuzi Changamoto mbalimbali zinazoikabili Taasisi.

***Wananchi wanapata
vyeti nya kuzaliwa
ndani ya Siku 7
tofauti na zamani
ilipokuwa ikichukua
zaidi ya miezi mitatu***

